# Ununuzi wa dawa jijini Dar es Salaam

## Je, maduka ya dawa yanazingatia kanuni?

## Utangulizi

Je, dawa zinaweza kutufanya wagonjwa? Je, zinatolewa ipasavyo? Na je, mfumo wa kuwalinda wananchi kutokana na madhara ya matumizi mabaya ya dawa unafanya kazi vizuri? Ili kujibu maswali haya, Youth Initiatives Tanzania (YITA), kwa kushirikiana na Twaweza, walifanya utafiti kuchunguza iwapo maduka ya dawa yanazingatia kanuni na taratibu zilizowekwa kusimamia uuzaji wa dawa kwa wateja. Zoezi hili lilifanyika mwezi Novemba 2011 kupitia utafiti katika maduka ya dawa jijini Dar es Salaam kwa kuwatumia “wateja siri”.

Muhtasari huu unaeleza yale yaliyojiri katika “ziara za siri” za utafiti. Unaonyesha kwamba, kinyume na kanuni zilizowekwa, maduka mengi ya dawa yanawauzia wateja dawa zinazopaswa kutolewa kwa agizo la daktari tu bila wateja kuwa na agizo hilo. Hali hii inaibua maswali kuhusu jinsi biashara ya kuuza dawa inavyosimamiwa nchini Tanzania, na iwapo afya za watu zinalindwa ipasavyo.

Kupitia shughuli ya kuuza dawa na vifaa vingine vya tiba, maduka ya dawa yanatoa huduma muhimu ya afya. Maduka ya dawa yanauza aina mbili za dawa: dawa zinazopaswa kutolewa kwa maagizo ya daktari (*prescription drugs*), ambazo zinaweza kuuziwa mgonjwa/mnunuzi iwapo tu ataonyesha agizo la dawa lililoandikwa na daktari, na dawa zinazoweza kuuzwa dukani hapo wakati wowote na hazihitaji kuonyesha agizo la dawa lililoandikwa na daktari.

Muhtasari huu umendaliwa na YITA kwa ushirikiano na Twaweza iliyopo Hivos Tanzania.

YITA, S.L.P 90540, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 240 1426.
Baruapepe: info@yita.org. Tovuti: www.yita.org

Aina ya kwanza inaweza kuleta madhara makubwa inapotumiwa vibaya, na ndio sababu agizo la dawa toka kwa daktari linatakiwa kabla dawa haijatolewa. Kununua na kutumia dawa zinazopaswa kuagizwa matumizi yake na daktari bila kibali cha daktari huweza kudhuru na hata kugeuka sumu kwa mtumiaji (kwa mfano, wagonjwa wanapotumia dawa zisizo sahihi au wanapotumia dawa katika vipimo visivyo sahihi) vilevile huweza kudhuru afya za watumiaji kwa namna nyingine (kwa mfano, kusababisha ugonjwa kuwa sugu na hivyo dawa kushindwa kutibu tatizo).

> *'Hakuna mtoaji dawa yeyote atakayetoa dawa ambazo matumizi yake yanapaswa kuwa kwa maagizo ya daktari tu isipokuwa kwa agizo la matumizi ya dawa husika lililotolewa na mfanyakazi wa afya, mganga wa meno au wa mifugo au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kuagiza matumizi ya dawa'*
>
> *The Tanzanian Food, Drugs and Cosmetics (Pharmaceutical Business Standards) Regulations, 2006: Kifungu cha 31; 3 (Tafsiri yetu)*

Ili kuzuia matumizi mabaya ya dawa, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania ((TFDA[1], www.tfda.or.tz), iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imepewa dhamana ya kusimamia ubora, usalama na ufanisi wa matumizi ya chakula na dawa. TFDA inaweka kanuni za kulinda afya za watu wanapotumia dawa; kanuni ambazo zinapaswa kuzingatiwa na maduka ya kuuza dawa. Ili yaweze kufanya kazi nchini maduka yote ya kuuza dawa yanapaswa kusajiliwa na TFDA na duka lolote halipaswi kuuza dawa zinazotakiwa kutumika kwa agizo la daktari kwa mgonjwa au mnunuzi asiyekuwa na agizo hilo kutoka kwa mfanyakazi wa afya aliyeidhinishwa (daktari).

## Mbinu za utafiti

Utafiti ulifanyika Novemba 2011 na ulihusisha watafiti waliofanya "ziara siri" 126 katika maduka 64 ya dawa katika wilaya tatu za Dar es Salaam: Ilala, Kinondoni na Temeke. Katika wilaya ya Ilala, maduka ya dawa yaliyotembelewa yalikuwa katika eneo la biashara la katikati ya mji na Kariakoo. Katika wilaya ya Kinondoni, "wateja siri " (watafiti) walitembelea maduka ya dawa yaliyopo Kinondoni, Magomeni, Manzese, Masaki, Msasani, Mwananyamala, Mwenge, Namanga, eneo la Savei/Mlimani City na Sinza. Wilayani Temeke, walitembelea maduka ya dawa yaliyopo Chango'mbe, Kigamboni na Temeke. Katika kila eneo maduka kadhaa yalitembelewa, mengi kati yao yakiwa katika maeneo yenye watu wengi.

Watafiti walikuwa wanawake watatu vijana, kila mmoja alikuwa na elimu ya shahada ya kwanza au stashahada. Watafiti hawa walitembelea maduka ya dawa yaliyochaguliwa kinasibu kutoka katika orodha ya utabibu (*Tanzania Medical Directory*, http://tanzaniamedicaldirectory.com/html/list.html). Mwanzoni,

1 *Tanzania Food and Drug Authority*

maduka ya dawa 64 kutoka 264 (asilimia 24) yaliyokuwa yameorodheshwa yalichaguliwa kushiriki. Hata hivyo, watafiti walipobaini katika siku yao ya kwanza ya ufuatiliaji kwamba maduka ya dawa mengi yaliyokuwa katika orodha hiyo hayakuwepo katika maeneo yaliyoorodheshwa, walitembelea maduka mengine mbadala katika maeneo hayo hayo. Maduka mbadala mengi hayakuwa yameorodheshwa katika *Tanzania Medical Directory*. Kiambatisho 1 kinaonyesha idadi ya maduka ya dawa yaliyotembelewa katika kila eneo na idadi ya ziara zilizofanywa katika eneo.

"Ziara siri" kwenye maduka ya dawa zilifanywa kwa namna mbili. Namna ya kwanza (ziara 88) ilihusisha mtafiti (wateja siri) kuingia dukani na kuomba kupata aina fulani ya dawa ambayo kwa mujibu wa kanuni ingepatikana kwa kuonyesha agizo la dawa kutoka kwa daktari. Namna ya pili, (ziara 38) ilihusisha mtafiti kumweleza mhudumu katika duka la dawa ugonjwa/dalili za ugonjwa wake au za mwanafamilia yake, na kutaka ushauri kuhusu aina ya dawa inayofaa anunue. Watafiti walishauriwa kusisitiza kupatiwa dawa—kama watu wafanyavyo katika hali ya kawaida—iwapo wahudumu wangekataa kutoa dawa baada ya ombi lao la kwanza.

Maongezi baina ya wahudumu katika maduka ya dawa na watafiti yalirekodiwa kwa uangalifu, na risiti na dawa zilizonunuliwa zilipigwa picha kwa utaratibu makini na yote kuwekwa katika kumbukumbu. Katika picha zinazoonekana hapa chini majina ya maduka katika risiti yamefichwa kuepuka kuonyesha duka husika.

## Mambo matatu kuonyesha iwapo dawa zinazopaswa kutolewa kwa agizo la daktari zinauzwa ipasavyo

### Jambo la 1: Katika asilimia 93 ya ziara 88, dawa zinazopaswa kutolewa kwa agizo la daktari ziliuzwa bila agizo kuwepo

Katika ziara 88 zilizofanywa katika maduka ya dawa, watafiti waliingia dukani na moja kwa moja kuulizia kununua aina fulani ya dawa inayohitaji mteja aonyeshe agizo la dawa lililoandikwa na daktari bila kuonyesha agizo hilo. Katika ziara 82 kati ya ziara za aina hiyo (asilimia 93), wahudumu waliuza dawa zilizotakiwa na wateja bila kuulizia agizo la daktari.

**Kielelezo cha 1: Dawa zinazohitaji kuonyesha agizo la dawa lililoandikwa na daktari zilizouzwa bila kuonyesha agizo hilo wakati mteja alipohitaji (%)**




**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011**

## Jambo la 2: Katika asilimia 92 ya ziara 38, dawa zinazohitaji agizo la daktari ziliuzwa baada ya mteja kueleza dalili za ugonjwa

Katika ziara 38 watafiti waliomba ushauri kutoka kwa wahudumu baada ya kuzungumza nao juu ya ugonjwa na/au dalili za ugonjwa wao. Katika ziara 35 kati ya ziara hizo 38 (asilimia 92), badala ya mhudumu kumshauri mgonjwa akamwone daktari kwanza, mhudumu alimshauri mteja kutumia dawa aina fulani, ambazo zingepaswa kutolewa tu baada ya kuonyesha agizo la dawa lililoandikwa na daktari, na kumuuzia dawa hizo.

**Kielelezo cha 2: Dawa zinazohitaji kuonyesha agizo la dawa lililoandikwa na daktari zinauzwa kwa wateja wanaoomba ushauri dukani bila kumwona daktari kwanza (%)**




**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011**

**Sanduku 1: Mfano wa mazungumzo ambapo mteja anaeleza tatizo lake na kuomba ushauri**

*'Nilimwambia mfamasia kwamba nina uambukizo kwenye njia ya mkojo na nilimwuliza ni aina gani ya dawa anafikiri itautibu ugonjwa huo. Alikwenda kwenye tarakilishi yake na kuandika kitu fulani. Baada ya kuandika alinigeukia na kusema, "Ni shilingi 7,500" Kisha nikamwuliza, "Jina la dawa hiyo ni nini?" Alinigeuzia skrini ya tarakilishi ili niweze kusoma jina. Nilisoma na kumwuliza iwapo atanipa risiti kama nitanunua dawa. Akasema, ndiyo'.*

**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011**

Kwa ujumla katika ziara 117 kati ya 126 (asilimia 93), dawa zilizohitaji mteja kuwa na agizo la dawa kutoka kwa daktari ziliuzwa bila mhudumu dukani kuulizia agizo hilo. Ni mara tisa tu (asilimia 7) ambapo wateja walikataliwa kuuziwa dawa kwa kushindwa kuonyesha agizo la daktari. Kielelezo cha 3 kinaonyesha mifano ya dawa zilizonunuliwa/kuuzwa bila kuzingatia kanuni za uuzaji dawa na risiti zilizotolewa

.

**Kielelezo cha 3: Mifano ya dawa zinazopaswa kuuzwa kwa agizo la dawa lililoandikwa na daktari lakini zilizouzwa bila kuonyesha agizo, na risiti**

**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011**

### Jambo la 3: Asilimia 100 ya maduka ya dawa katika maeneo 12 kati ya 15 yaliyotembelewa yaliuza dawa kinyume cha kanuni

Kwa ujumla ilikuwa rahisi kupata dawa zinazohitaji agizo la dawa kutoka kwa daktari karibu katika nyakati zote, isipokuwa katika maeneo machache tu. Katika maeneo 12 kati ya 15 yaliyotembelewa, watafiti waliweza kupata dawa hizo bila kuonyesha agizo la dawa liloandikwa na daktari katika asilimia 100 ya ziara walizofanya (Kielelezo cha 5). Ni katika maeneo matatu tu (Masaki, Eneo la biashara la katikati ya mji, na Savei/Mlimani City) ndiko watafiti walinyimwa dawa hizo kwa kutokuwa na agizo kutoka kwa daktari, na pia ni katika baadhi tu ya ziara zao katika maeneo hayo.

**Kielelezo cha 5: Dawa zinazopaswa kutolewa baada ya kuonyesha agizo la dawa liloandikwa na daktari zilizouzwa bila kuonyesha agizo hilo, kwa eneo**




**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011**

## Hitimisho

Muhtasari huu umewasilisha matokeo ya zoezi la ufuatiliaji ambalo lilitaka kufahamu ni kwa kiasi gani maduka ya dawa jijini Dar es Salaam yanazingatia kanuni zilizowekwa na TFDA kuhusu uuzaji wa dawa zinazopaswa kutolewa kwa agizo la daktari.

Utafiti, ulioendeshwa na YITA kwa ushirikiano na Twaweza mwezi Novemba 2011, uligundua kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa kanuni zilizowekwa. Karibu katika ziara zote (asilimia 93), maduka ya dawa jijini Dar es Salaam yaliuza dawa zinazohitaji agizo la daktari bila kufuata utaratibu. Taarifa kadhaa za "wateja siri" pia zinaonyesha kuwa wahudumu katika maduka ya dawa wanaweza kushawishiwa na wateja kwa urahisi kuwauzia dawa bila kuonyesha agizo la daktari.

Katika njia zote mbili zilizotumiwa na watafiti–iwapo mteja aliulizia dawa kwa kuitaja jina au aliomba ushauri ili kutibu tatizo lake fulani la afya, matokeo ni yale yale. Ni wazi kwamba kanuni za TFDA za utoaji dawa zinakiukwa mara nyingi jijini Dar es Salaam na kwamba mfumo wa kusimamia kanuni zilizowekwa haufanyi kazi.

- Matokeo yake ni kwamba kwa kiasi kikubwa afya za wananchi zinawekwa katika mazingira hatarishi. Hii ni pamoja na:
- Uwezekano wa wagonjwa kutumia dawa katika vipimo visivyo sahihi ambavyo vinaweza kusababisha dawa kushindwa kutibu tatizo lao na kusababisha pia matatizo mengine, ikiwa ni pamoja na dawa kuwa sumu mwilini;
- Wagonjwa wanaweza kuishia kutumia dawa zisizo sahihi kwa matatizo ya kiafya waliyo nayo na hivyo kuziweka afya zao hatarini;

Wagonjwa wanaweza kujenga utegemezi kwa dawa fulani.

Zoezi hili la ufuatiliaji halikuchunguza sababu za tatizo hili kuenea kwa kiasi kikubwa hivyo, lakini mtu anaweza kukisia. Je, inawezekana kwamba wahudumu katika maduka ya dawa hawajapata mafunzo ya kutosha na hawana uelewa? Au wana uelewa lakini msukumo toka kwa wamiliki kupata faida, ukichanganywa na mfumo hafifu wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa kanuni vinawafanya wapuuze maarifa waliyonayo na kuuza dawa bila kuzingatia kanuni? Au msukumo mkubwa wa hali hii unatokana na matarajio ya wananchi wenyewe ya kupata dawa kwa haraka na urahisi, bila gharama kubwa, bila shida na wakati mwingine bila unyanyasaji wanaofanyiwa wakiwa mikononi mwa wahudumu wa afya?

Hatujui kwa hakika majibu ya maswali haya. Lakini iwapo tunajali kuhusu afya na hali bora za watu, kushughulikiwa kwa maswali haya na kutafuta ufumbuzi unaofaa ni jambo la msingi linalopaswa kufanywa na TFDA, Wizara ya Afya na wananchi kadhalika.

**Kiambatisho 1: Maduka ya dawa yaliyotembelewa na tabia ya uuzaji dawa**

| Eneo | Idadi ya maduka ya dawa yaliyote-mbelewa | Idadi ya ziara za siri | Dawa zilizouzwa bila kuonyesha agizo la daktari | Dawa ambazo hazikuuzwa bila kuonyesha agizo la daktari | Dawa zilizouzwa bila kuonyesha agizo la daktari (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Kariakoo | 11 | 22 | 22 | 0 | 100% |
| Magomeni | 4 | 8 | 8 | 0 | 100% |
| Manzese | 3 | 6 | 6 | 0 | 100% |
| Masaki | 3 | 4 | 2 | 2 | 50% |
| Msasani | 4 | 8 | 8 | 0 | 100% |
| Namanga | 2 | 4 | 4 | 0 | 100% |
| Eneo la Biashara la Katikati ya mji | 9 | 18 | 14 | 4 | 78% |
| Kigamboni | 2 | 4 | 4 | 0 | 100% |
| Mwananyamala | 4 | 8 | 8 | 0 | 100% |
| Kinondoni | 5 | 10 | 10 | 0 | 100% |
| Sinza | 5 | 9 | 9 | 0 | 100% |
| Mwenge | 4 | 8 | 8 | 0 | 100% |
| Eneo la Savei/Mlimani City | 2 | 4 | 1 | 3 | 25% |
| Temeke | 4 | 8 | 8 | 0 | 100% |
| Chang'ombe | 2 | 5 | 5 | 0 | 100% |
| **Jumla** | **64** | **126** | **117** | **9** | **93%** |

**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011.**

**Kumbuka:** Duka moja tu katika kila eneo ndilo lilitembelewa katika maeneo ya Savei/Mlimani City. Ziara za siri mbili zilifanywa katika kila duka.

**Kiambatisho 2: Idadi ya ziara na dawa zilizotolewa**

| **Jumla ya ziara** | **126** |
|---|---|
| Dawa ziliuzwa zilipotakiwa | 82 |
| Dawa hazikuuzwa zilipotakiwa | 6 |
| Dawa ziliuzwa baada ya kuomba ushauri | 35 |
| Dawa hazikuuzwa baada ya kuomba ushauri | 3 |

**Chanzo: YITA Pharmacy Survey, 2011.**